رئاسة الشؤون الدينية
بالمسجد الحرام والمسجد النبوي

# NAMNA YA SWALA YA MTUME (REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE)

Kiswahili

سواحيلي

كيفية صلاة النبي صلى الله عليه وسلم


**Mwandishi**

Mheshimiwa, Sheikh

Abdul-‘Azīz bin Abdillah bin Baaz

# كيفية صلاة النبي

## صلى الله عليه وسلم

# NAMNA YA SWALA YA MTUME (REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE)

**(Kwa Kiswahili)**


**Mwandishi**

Mheshimiwa, Sheikh

Abdul-‘Azīz bin Abdillah bin Baaz

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.

Kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu pekee, na rehema na amani ziwe juu ya mja wake na mtume wake, nabii wetu Muhammadi na watu wake na Maswahaba zake, ama baada hayo:-

Haya ni maneno mafupi katika kubainisha namna ya swala ya Mtume, nimetaka kuyaweka mbele ya kila Muislamu wa kiume na Muislamu wa kike, ili kila anayeisoma, ajitahidi kumuiga katika hilo, kwa mujibu wa kauli yake: "Swalini kama mlivyoniona mimi nikiswali."[1] (Kaipokea Bukhari). Na kwa msomaji, sasa huu ndio ufafanuzi wa hilo:

## Kueneza maji ya Udhu sawasawa

1. Ataeneza sawasawa maji ya udhu, na hilo ni mtu atawadhe kama alivyoamrishwa na Mwenyezi Mungu; kwa kuifanyia kazi kauli yake aliyetakasika na kutukuka:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قُمۡتُمۡ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغۡسِلُواْ وُجُوهَكُمۡ وَأَيۡدِيَكُمۡ إِلَى ٱلۡمَرَافِقِ وَٱمۡسَحُواْ بِرُءُوسِكُمۡ وَأَرۡجُلَكُمۡ إِلَى ٱلۡكَعۡبَيۡنِۚ﴾. المائدة، الآية (6).

"Enyi mlioamini, pindi mtakaposimama kutaka kuswali, basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka katika viwiko, na pakeni maji vichwa vyenu, (na muoshe) miguu yenu mpaka katika fundo mbili."[2] Mpaka mwisho wa Aya.

---

(1) Kaipokea Bukhari, Adhana (605), na Ad-Daarimi, Swala (1253).
(2) Al-Maidah, aya ya 6.

Na kauli yake Mtume: "Haikubaliki swala pasina twahara."[3]

## Kuelekea Kibla

2. Mwenye kuswali anatakiwa aelekee Kibla, nayo ni Al-Kaaba, mahala popote atakapokuwa kwa mwili wake wote akiwa amekusudia kwa moyo wake kufanya ibada ya swala anayoikusudia kama vile swala ya faradhi au sunna. Asiitamke nia kwa ulimi wake; kwa sababu kutamka kwa ulimi si katika sheria, bali ni uzushi. Kwa sababu, Mtume hakuitamka nia, wala Maswahaba zake, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao. Anatakiwa aweke kizuizi mbele yake atakachoswali huku amekielekea akiwa ni imamu au peke yake. Kuelekea Kibla ni sharti katika swala isipokuwa katika baadhi ya maswala machache yanayofahamika, na yamewekwa wazi katika vitabu vya wanachuoni.

## Takbira ya kuhirimia swala na kunyanyua mikono wakati wa takbira, na kuweka mikono miwili juu ya kifua

3. Atatoa takbira ya kuhirimia swala kwa kusema: "*Allaahu Akbaru*", huku macho yake yakitazama mahala pake pa kusujudu.

4. Atanyanyua mikono yake wakati wa takbira mpaka usawa wa mabega yake au usawa wa masikio yake.

5. Ataweka mikono yake juu ya kifua chake, mkono wa kulia ukiwa juu ya kiganja chake cha kushoto na kiwiko na muundi wa mkono, kwa sababu hili limethibiti kutoka kwa Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

---

(3) Muslim, Twahara (224), At-Tirmidhi, Twahara (1), Ibn Maajah, Twahara na sunna zake (272), Ahmad (2/73).

## Dua ya ufunguzi wa swala

6. Ni sunna mtu asome dua ya ufunguzi wa swala, nayo ni: *"Allaahumma baaid, bainii wabaina khatwaayaaya, kamaa baa'atta bainal Mashriqi wal Maghribi. Allaahumma naqqinii min khatwaayaaya kamaa yunaqqath-thaubul abyadhu minad-danasi. Allaahummaghsil-nii min khatwaayaaya bil-maai wath-thalji wal-baradi."* Maana yake: (Ewe Mwenyezi Mungu, weka mbali kati yangu mimi na makosa yangu kama ulivyoweka mbali kati ya Mashariki na Magharibi. Ewe Mwenyezi Mungu, nitakase mimi kutokana na makosa, kama ambavyo hutakaswa nguo nyeupe kutokana na uchafu. Ewe Mwenyezi Mungu, nioshe mimi kutokana na makosa yangu kwa maji na theluji na baridi). Na akitaka, anaweza kusema badala ya dua hiyo: *"Sub-haanaka llaahumma wabihamdika, watabaarakas-muka, wata'aala jadduka walaa ilaaha ghairuka."* Maana yake: (Umetakasika ewe Mwenyezi Mungu, na sifa njema ni zako, na limetukuka jina lako, na umetukuka ufalme wako, na hakuna mungu zaidi yako).[4] Na akisoma dua zingine zisizokuwa hizo, miongoni mwa zile zilizothibiti kutoka kwa Mtume, pia hakuna ubaya. Na kilicho bora zaidi ni asome dua hii wakati mwingine na dua hii wakati mwingine, kwa sababu hilo ndilo linamtia katika ukamilifu zaidi wa kumfuata Mtume. Kisha atasema: *"A'udhu billahi minashshaytwaanir-rajiim."* Maana yake: (Ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na Shetani aliyelaaniwa). Kisha aseme: *"Bismillahir-rahmanir-rahiim."* Maana yake: (Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye

(4) Bukhari, Adhana (711), Muslim, Misikiti na sehemu za swala (598), An-Nasaai, Ufunguzi wa swala (895), Abuu Daudi, Swala (781), Ibn Maajah, Kusimamisha swala na Sunna zake (805), Ahmad (2/231), Ad-Daarimi, Swala (1244).

kurehemu). Kisha asome Suratul-Faatiha, kwa mujibu wa kauli yake: "Hakuna swala kwa ambaye hatosoma ufunguzi wa kitabu (Suratul-Faatiha)."[(5)].

Na atasema: "*Aaamiiin*" baada yake, yaani: 'Ewe Mwenyezi Mungu pokea dua', kwa sauti kubwa katika swala za sauti kubwa, na kwa siri katika swala za siri. Kisha atasoma kiasi anachokiweza katika Qur'ani. Kilicho bora zaidi ni asomesura fupi za kati na kati baada ya Suratul-Faatiha, katika swala ya Adhuhuri, Laasiri na Ishaa. Na katika swala ya Al-fajiri asome sura ndefu. Na katika swala ya Maghribi, saa nyingine asome sura ndefu, na wakati mwingine sura fupi; kwa kuzifanyia kazi hadithi zilizokuja kulieleza hilo.

## Kurukuu na kunyanyuka kutoka katika rukuu na yanayoambatana nayo

7. Atanyanyuka huku akitoa takbira, na huku akinyanyua mikono yake mpaka usawa wa mabega yake au masikio yake. Atakiweka kichwa chake usawa wa mgongo wake na huku ameweka mikono yake juu ya magoti yake kwa kuvisambaza vidole vyake. Atulizane katika rukuu yake na aseme: "*Sub-haana Rabbiyal-Adhwiim*" Maana yake: Umetakasika Mola wangu Mlezi, Mtukufu. Na bora zaidi ni airudie dua hii mara tatu au zaidi. Pia inapendekezwa kusema pamoja na hivyo: *"Sub-haanaka llaahumma wabihamdika. Allaahumma*

---

(5) Bukhari, Adhana (723), Muslim, Swala (394), At-Tirmidhi, Swala (247) An-Nasaai, Ufunguzi wa swala (911), Abuu Daudi, Swala (822), Ibn Maajah, Kusimamisha swala na Sunna zake (837), Ahmad (2/316), Ad-Daarimi, Swala (1242).

*ghfirlii."* Maana yake: Umetakasika ewe Mwenyezi Mungu, na sifa njema ni zako. Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe.(6)

8. Atanyanyua kichwa chake kutoka katika rukuu huku amenyanyua mikono yake mpaka usawa wa mabega yake au masikio yake huku akisema: *"Sami'allaahu liman hamidah"* Yaani: Amemsikia Mwenyezi Mungu mwenye kumhimidi.(7) Na hili ni endapo atakuwa imamu au wakati anaswali peke yake. Na atasema wakati wa kunyanyuka kwake: *"Rabbanaa walakal-hamdu, hamdan kathiiran twayyiban, mubaarakan fiihi. Mil-ass-samaawaati, wamil-al-ardhwi, wamil-amaa baina humaa, wamil- amaa shi ita min shai-in baad."* Yaani: Ewe Mola wetu Mlezi, unastahiki sifa njema, sifa nyingi, nzuri, zenye baraka, kwa ujazo wa mbingu, na ujazo wa Ardhi, na ujazo wa vilivyo kati yake, na ujazo wa chochote utakacho baada yake."(8) Ama akiwa nyuma ya imamu (maamuma), basi atatakiwa kusema wakati wa kunyanyuka: *'Rabbanaa walakal-hamdu'*, yaani (Ewe Mola wetu Mlezi, ni zako sifa njema zote) mpaka mwisho wa maneno yaliyotangulia. Na endapo atazidisha kila mmoja wao, ninakusudia imamu na maamuma na anayeswali peke yake: *"Ahluth'thanaa walmajd, ahaqqu maaqaalal 'abdu, wakulluna laka 'abdu. Allahumma laa maania limaa a'atwaita, walaa mu'utwiya limaa mana'ata, walaa yanfa'u dhaljaddi minkal jaddu."*

---

(6) Bukhari, Tafsiri ya Qur'ani (4683), Muslim, Kitabu cha swala (484), An-Nasaai, Tatbiiq (1122), Abuu Daudi, Swala (877), Ibn Maajah,Kusimamisha swala na Sunna zake (889).

(7) Bukhari, Adhana (657), Muslim, Swala (411) At-Tirmidhi, Swala (361), An-Nasaai, Imaama (832), Abuu Daud, Swala (601), Ibn Maajah, Kusimamisha swalaa na sunna zake (1238), Imam Malik, Kuita kwenye swalaa (306), Ad-Daarimi, Swala (1256).

(8) Muslim, Swala ya wasafiri na kuipunguza (771), At-Tirmidhi, Dua mbalimbali (3423), Abuu Daud, Swala (760), Ahmad (1/103).

Yaani: Unastahiki zaidi sifa njema na utukufu, haya ni maneno ya haki zaidi aliyoyasema mja, nasi sote ni waja wako. Ewe Mwenyezi Mungu, hakuna wa kuzuia uliyoyatoa, wala wa kuyatoa uliyoyazuia, wala hawezi kunufaisha mwenye utukufu (yeyote) kuliko wewe ewe Mtukufu.[(9)] Basi itapendeza zaidi kwa sababu hilo limethibiti kutoka kwake, na inapendekezwa kwamba kila mmoja miongoni mwao aweke mikono yake juu ya kifua chake kama alivyofanya katika kusimama kwake kabla ya kurukuu, kwa sababu ya kuthibiti yenye kuonyesha hilo kutoka kwa Mtume, kutoka kwa hadithi ya Wail bin Hujari na Sahli, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

## Kusujudu na kunyanyuka kutoka katika sijida na yanayoambatana nayo

9. Atasujudu huku akitoa takbira, kwa kuweka magoti yake kabla ya mikono yake ikiwa itakuwa rahisi kwake kufanya hivyo. Lakini ikiwa ni vigumu kwake, basi atatanguliza mikono yake kabla ya magoti yake, akiwa kaelekea Kibla kwa vidole vya miguu yake na mikono yake, akiwa kavifungamanisha vidole vya mikono yake huku kavinyoosha, na atakuwa juu ya viungo vyake saba: Paji la uso pamoja pamoja na pua, mikono miwili, magoti mawili na tumbo za vidole vya miguu miwili. Atasema: *"Sub-haana Rabbiyal-A'alaa."* Yaani: 'Ametakasika Mola wangu Mlezi aliye juu zaidi.' Ni sunna aseme hivyo mara tatu au zaidi, na inapendekezwa aseme pia pamoja na hivyo: *"Sub-haanaka llaahumma rabbanaa wabihamdika. Allaahumma ghfirli."* Yaani: Umetakasika ewe Mwenyezi Mungu, Mola wetu Mlezi, na sifa njema ni zako. Ewe Mwenyezi Mungu,

---

(9) Muslim, Swala (477), An-Nasaai, Tatbiiq (1068), Abuu Daud, Swala (847), Ahmad (3/87) Ad-Daarimi, Swala (1313).

nisamehe.(10) Na hapo azidishe kuomba dua kwa mujibu wa kauli ya Mtume: "Ama katika rukuu, mtukuzeni sana Mola Mlezi. Na ama katika sijida, jitahidini sana kuomba dua kwa wingi. Kwani hapo ni mahala bora zaidi kwenu nyinyi pa kujibiwa dua."(11) Na hapo atamuomba Mola wake Mlezi katika kheri za Dunia na Akhera, sawa sawa swala iwe ni ya faradhi au ya sunna. Na atatanua mikono yake iwe mbali na mbavu zake, na tumbo lake liwe mbali na mapaja yake, na mapaja yake yawe mbali na miundi yake. Atanyanyua dhiraa (mikono) yake isilale juu ya Ardhi, kwa mujibu wa kauli ya Mtume: "Linganeni sawa katika sijida, na asitandaze mmoja wenu mikono yake kama anavyoitandaza mbwa."(12)

## Kukaa baina ya sijida mbili na namna yake

10. Atanyanyua kichwa chake huku akitoa takbira, na atatandika mguu wake wa kushoto na kuukalia, na atasimamisha mguu wake wa kulia na ataweka mikono yake juu ya mapaja yake na magoti yake, na atasema: *"Rabbighfirlii war-hamnii wahdinii warzuqunii waafinii waj-burnii."* Ewe Mola wangu Mlezi, nisamehe na unirehemu, na uniongoze, na uniruzuku, na unipe salama na uniunge.(13) Na atatulizana katika kikao hiki.

---

(10) Bukhari, Adhana (761) Muslim, Swala (484), An-Nasaai, Tatbiiq (1122), Abuu Daud, Swala (877), Ibn Maajah, Kusimamisha swala na sunna zake (889), Ahmad (6/43).

(11) Muslim, Swala (479), An-Nasaai, Tatbiiq (1120), Abuu Daud, Swala (876), Ahmad (1/219) Ad-Daarimi, Swala (1325).

(12) Bukhari, Adhana (788), Muslim, Swala (493), Ahmad (3/192).

(13) At-Tirmidhi, Swalaa (284), Abuu Daud, Swalaa (850), Ibn Maajah, Kusimamisha swalaa na sunna zake (898).

11. Atasujudu sijida ya pili huku akitoa takbira na atafanya ndani yake kama alivyofanya katika sijida ya kwanza.

12. Atanyanyua kichwa chake huku akitoa takbira, na atakaa kikao kifupi kama kikao cha kati ya sijida mbili. Kikao hiki kinaitwa kikao cha mapumziko. Nacho si cha lazima, bali kinapendekezwa tu, na hata akikiacha, basi hakuna ubaya juu yake. Kikao hiki hakina dhikri wala dua yoyote. Kisha atanyanyuka juu kwa ajili ya rakaa ya pili kwa kuegemea magoti yake ikiwa hilo litakuwa jepesi kwake. Na kama litakuwa gumu kwake, basi atajitegemeza kwenye Ardhi. Kisha atasoma Faatiha na chochote kilicho chepesi kwake katika Qur'ani baada ya Faatiha. Kisha atafanya kama alivyofanya katika rakaa ya kwanza.

## Kukaa kwa ajili ya Tahiyatu katika swala yenye rakaa mbili na namna yake

13. Swala itakapokuwa na rakaa mbili kama vile swala ya Alfajiri, Ijumaa na Idi mbili, basi atakaa baada ya kunyanyuka kwake kutoka katika sijida ya pili akiwa kausimamisha mguu wake wa kulia, na kautandika mguu wake wa kushoto, huku kauweka mkono wake wa kulia juu ya paja lake la kulia, akiwa kavikunja vidole vyake vyote, isipokuwa kidole cha shahada. Atakinyoosha kwa kuashiria kumpwekesha Mwenyezi Mungu. Na akikunja kidole kidogo cha mwisho cha mkono wake wa kulia na kile kinachofauatia, na akatengeneza duara kwa kidole cha kati na kidole gumba na akanyoosha kidole cha shahada, basi ni vizuri pia, kwa sababu hizi sifa mbili zote zilithibiti kutoka kwa Mtume, na kilicho bora zaidi ni afanye hili wakati mwingine na wakati mwingine hili. Atauweka mkono wake wa kushoto juu ya paja lake la kushoto na goti lake,

kisha atasoma tahiyatu katika kikao hiki, nayo ni: *"Attahiyyaatulillahi, wasswalawaatu wattwayyibaatu. Assalaamu 'alaika ayyuhan-nabiyyu warahmatullahi wabarakaatuhu. Assalaamu 'alaina, wa'alaa 'ibadillahis-swaalihiina. Ash-hadu an-laailaaha illa llahu wa ashhadu anna Muhammadan 'abduhu warasuuluhu" Kisha atasema: Allahumma swalli 'alaa Muhammadin wa'alaa aali Muhammadi. Kamaa swallaita 'alaa Ibrahiima wa'alaa aali Ibrahiima. Innaka hamiidun majiid. Allahumma baariki 'alaa Muhammadin wa 'alaa aali Muhammadin, kamaa baarakta 'alaa Ibrahiima wa- 'alaa aali Ibrahiima. Innaka hamiidun majiid."* Tafsiri yake: Maamkizi ni ya Mwenyezi Mungu, na swala na vyote vilivyo vizuri. Amani iwe juu yako, ewe Nabii na rehema ya Mwenyezi Mungu na baraka zake. Amani iwe juu yetu na juu ya waja wema wa Mwenyezi Mungu. Ninashuhudia kuwa hapana mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ninashuhudia kuwa Muhammadi ni mja wake na ni Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu, mpe rehema Muhammad na watu wa familia ya Muhammad, kama ulivyompa rehema Ibrahim na watu wa familia ya Ibrahim. Hakika Wewe ni Msifiwa, Mwenye utukufu. Ewe Mwenyezi Mungu, mbariki Muhammad pamoja na watu wa familia ya Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na watu wa familia ya Ibrahim. Hakika Wewe ni Msifiwa, Mwenye utukufu.(14) Na atajikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na mambo manne, atasema: *"Allaahumma inni a'udhubika min 'adhaabi jahannama, wa min 'adhaabil qabri, wamin fitnatil mahyaa wal mamaati, wamin sharri fitnatil masiihiddajjaali."* Maana yake: ‘Ewe

---

(14) Bukhari, Adhana (797), Muslim, Swala (402), At-Tirmidhi, Ndoa (1105) An-Nasaai, Kusahau (1298), Abuu Daudi, Swala (968), Ibn Maajah, Kusimamisha swala na Sunna zake (899), Ahmad (1/428), Ad-Daarimi, Swala (1340).

Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajilinda kwako kutokana na adhabu za Jahanamu, na majaribu ya uhai na ya kifo, na kutokana na majaribu ya Masihi Dajali.' (Kaipokea Muslim).[15] Kisha ataomba chochote akitakacho katika kheri za dunia na Akhera. Na akiwaombea wazazi au wengineo miongoni mwa Waislamu, pia hakuna ubaya - sawa sawa swala iwe ni ya faradhi au sunna, kwa mujibu wa ujumla wa kauli ya Mtume katika hadithi ya Ibn Masudi wakati Mtume alipomfundisha Tahiyatu. Kisha atachagua katika dua zile azipendazo zaidi na ataomba kwa hizo. Na katika tamko jingine, *"Kisha achague katika maombi ayatakayo."* Hili linajumuisha yote yanayomnufaisha mja katika dunia na akhera. Kisha atoe salamu kuliani kwake na kushotoni kwake kwa kusema: *"Assalaam 'alaikum warahmatullaah. Assalaam 'alaikum warahmatullaah."* Maana yake: Amani iwe juu yenu, na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake. Amani iwe juu yenu, na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake.

## Kukaa kwa ajili ya tahiyatu katika swala yenye rakaa tatu au nne na namna yake

14. Endapo swala yake itakuwa ni ya rakaa tatu kama vile Maghribi, au rakaa nne kama vile Adhuhuri, Laasiri na Ishaa, atasoma tahiyatu iliyotajwa hapo awali pamoja na kumswalia Mtume. Kisha atanyanyuka asimame kwa kujitegemeza juu ya magoti yake, huku akinyanyua mikono yake usawa wa mabega yake au masikio yake huku akisema: *"Allaahu Akbaru",* (yaani 'Mwenyezi Mungu ni

(15) Bukhari, Jeneza (1311), Muslim, Misikiti na maeneo ya swala (588), At-Tirmidhi, Dua mbalimbali (3604) An-Nasaai, Kujikinga kwa Mwenyezi Mungu (5513), Abuu Daudi, Swala (983), Ibn Maajah, Kusimamisha swala na Sunna zake (983), Ahmad (2/454), Ad-Daarimi, Swala (1344).

Mkubwa'), na ataiweka (yaani mikono yake) juu ya kifua chake kama ilivyotangulia, na atasoma Faatiha pekee. Lakini ikiwa atasoma katika rakaa ya tatu na ya nne katika swala ya Adhuhuri na Laasiri zaidi ya suratul Faatiha katika baadhi ya nyakati, pia hakuna ubaya; kwa sababu yamethibiti yanayoashiria hilo kutoka kwa Mtume, katika hadithi ya Abuu Sa'idi. Kisha atakaa tahiyatu baada ya rakaa ya tatu ya swala ya Magharibi, na baada ya rakaa ya nne katika swala ya Adhuhuri, Laasiri na Ishaa, kama ilivyotangulia katika swala zenye rakaa mbili mbili. Kisha atatoa salamu kuliani kwake na kushotoni kwake, na atamtaka msamaha Mwenyezi Mungu mara tatu, kisha atasema: *"Allahumma antassalaam, waminkassalaam, tabaarakta yaa dhaljalaali wal ikraam."* Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu, hakika wewe ndiye amani, na amani hutoka kwako. Umetukuka ewe Mwenye utukufu na ukarimu.(16) Hili ni kabla ya kuwageukia watu kama atakuwa ni imamu. Kisha atasema: *"Laa ilaaha illa llaahu wahdahuu laa shariika lahu, lahul-mulku walahul-hamdu, wahuwa 'alaa kulli shai-in qadiir. Allaahumma laa maani'a limaa a'atwaita, walaa mu'utwiya limaa mana'ata, walaa yanfa'u dhal-jaddi minkal-jaddu. Laa haulaa walaa quwwata illaa billaah. Laa ilaaha illa llaahu walaa na'abudu illaa iyyahu, lahun-niimatu, walahul-fadhlu walahuth-thanaaul-hasan. Laa ilaaha illa llaahu mukhliswiina lahuddiin walau karihal kaafiruun."* Tafsiri: 'Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, yeye pekee asiye na mshirika, ufalme ni wake na sifa njema ni zake, naye ni Muweza mno wa kila kitu. Ewe Mwenyezi Mungu, hakuna wa kuyazuia uliyoyatoa, wala wa kuyatoa uliyoyazuia, na wala

---

(16) Muslim, Misikiti na maeneo ya swala (591), At-Tirmidhi, Swala (300), Abuu Daud, Swala (1512), Ibn Maajah, Kusimamisha swalaa na sunna zake (928), Ahmad (5/280), Ad-Daarimi, Swala (1348).

hawezi kunufaishwa mwenye utukufu kukuliko wewe ewe Mtukufu. Hapana uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu. Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na wala hatumuabudu yeyote ila Yeye. Yeye ndiye Mwenye neema, na fadhila zote ni zake, na Yeye ndiye Mwenye sifa nzuri. Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa tunamtakasia dini (matendo) hata kama makafiri watachukia.'[17] Na atamtakasa Mwenyezi Mungu kwa kusema: (*Sub-haanallaah*) mara thelathini na tatu, na amsifu kwa kusema: (*Alhamdulillaah*) mfano wa idadi hiyo, na amtukuze kwa kusema: (*Allaahu Akbaru*) kwa idadi hiyo. Kisha atasema ili kukamilisha mia moja: '*Laa ilaaha illa llaahu wahdahuu laa shariika lahu, lahulmulku walahul-hamdu wahuwa 'alaa kulli shai-in qadiir.*' Kisha atasoma ayatul Kursiy, Qul-huwallaahu ahad, Qul-audhubirabbil-falaq na Qul-audhubirabbin naasi, baada ya kila swala. Ni sunna kuzikariri sura hizi mara tatu tatu baada ya swala ya Alfajiri na swala ya Magharibi, kwa sababu kuna hadithi zilizosimulia hilo kutoka kwa Mtume. Nyiradi hizi zote ni sunna wala si faradhi.

Inaruhusika katika sheria kwa kila Muislamu wa kiume na wa kike kuswali kabla ya swala ya Adhuhuri rakaa nne na baada yake rakaa mbili. Na rakaa mbili baada ya swala ya Magharibi na Ishaa. Na rakaa mbili kabla ya swala ya Alfajiri. Hizi zote ni jumla ya rakaa kumi na mbili. Rakaa hizi huitwa *rawaatib* (sunna zilizopangiliwa na zenye malipo maalumu) kwa sababu Mtume alikuwa akidumu

---

(17) Bukhari, Adhana (808), Muslim, Misikiti na maeneo ya swala (593), An-Nasaai, Kusahau (1341), Abuu Daud, Swala (1505), Ahmad (4/250), Ad-Daarimi, Swala (1349).

kuziswali anapokuwa nyumbani. Ama safarini, alikuwa akiziacha isipokuwa sunna ya Alfajiri na witiri; kwani hizo, yeye rehema na amani ziwe juu yake alikuwa akizidumisha anapokuwa nyumbani na safarini. Na kilichobora zaidi ni ziswaliwe sunna hizi ndani ya nyumba. Lakini ikiwa ataziswalia msikitini, basi hakuna ubaya; kwa mujibu wa kauli ya Mtume: *"Swala bora zaidi kwa mtu ni ile ya nyumbani kwake isipokuwa swala ya faradhi."*[(18)] Na kudumisha rakaa hizi ni miongoni mwa sababu za kuingia Peponi, kwa kauli ya Mtume: *"Atakayeswali rakaa kumi na mbili katika mchana wake na usiku wake kwa hiari, basi Mwenyezi Mungu atamjengea nyumba Peponi."*[(19)] (Kaipokea Muslim katika sahihi yake).

Na ikiwa ataswali rakaa nne kabla ya Laasiri, rakaa mbili kabla ya swala ya Magharibi na akaa mbili kabla ya swala ya Ishaa, pia ni vizuri. Kwa sababu yamethibiti kwa njia sahihiyanayoonyesha hivyo kutoka kwa Mtume. Na Mwenyezi Mungu ndiye msimamizi wa kuwezesha, na rehema na amani ziwe juu ya Nabii wetu Muhammad bin Abdillah, na juu ya watu wa familia yake, Maswahaba zake na wote wanaomfuta kwa wema mpaka siku ya Malipo.

---

(18) Bukhari, Al-Adab (5762), Muslim, Swala ya wasafiri na kuipunguza (781), At-Tirmidhi, Swala (450), An-Nasaai, Kuswali usiku na kuswali mchana kwa hiari (1599), Abuu Daud, Swala (1447), Ahmad (5/186), Maaliki, Kuita kwenye swala (293), Ad-Daarimi, Swala (1366)

(19) Muslim, Swala ya wasafiri na kuipunguza (728), At-Tirmidhi, Swala (415), An-Nasaai, Kuswali usiku na kuswali mchana kwa hiari (1801), Abuu Daud, Swala (1250), Ibn Maajah, Kusimamisha swala na sunna zake (1141), Ahmad (6/327).

## Yaliyomo

Kueneza maji ya Udhu sawasawa ............................................ 2
Kuelekea Kibla ........................................................................3
Takbira ya kuhirimia swala na kunyanyua mikono wakati wa takbira, na kuweka mikono miwili juu ya kifua ..............................3
Dua ya ufunguzi wa swala ........................................................4
Kurukuu na kunyanyuka kutoka katika rukuu na yanayoambatana nayo.......................................................................................5
Kusujudu na kunyanyuka kutoka katika sijida na yanayoambatana nayo.......................................................................................7
Kukaa baina ya sijida mbili na namna yake...................................8
Kukaa kwa ajili ya Tahiyatu katika swala yenye rakaa mbili na namna yake ............................................................................9
Kukaa kwa ajili ya tahiyatu katika swala yenye rakaa tatu au nne na namna yake ..........................................................................11

رئاسة الشؤون الدينية
بالمسجد الحرام والمسجد النبوي